


## Dondoo za mpango wa

# KIMKAKATI WA LSF WA 2022-2026

## Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Maeneo shughuli zetu zinakofanyika | 03 |
| Dondoo za mpango huu | 04 |
| Lengo la mpango | 04 |
| Nguzo kuu za mpango huu | 05 |
| Dira na dhamira | 06 |
| Misingi inayotuongoza | 07 |
| Malengo makuu ya kimkakati | 08 |
| Mfumo wa kutathmini matokeo ya shughuli zetu | 09 |
| Nadharia ya mabadiliko | 09 |




# Maeneo shughuli zetu zinakofanyika

## Dondoo muhimu za Mpango wa Kimkakati wa LSF wa 2022-2026

Legal Services Facility (LSF) ilianzishwa mwaka 2011 kama mfuko wa ruzuku utakaotoa fedha kwa kuzingatia usawa wa fursa kwa asasi zinazotoa na kuwezesha upatikanaji wa haki nchini pamoja na huduma za msaada wa kisheria pamoja na wasaidizi wa kisheria Tanzania Bara na Zanzibar. LSF inalenga kukuza na kulinda haki za binadamu kwa wote, hususani kwa wanawake na makundi maalumu. Shirika hili pia linasaidia kukuza uwezo wa kitaasisi na kitaalamu wa watoa huduma za msaada wa kisheria pamoja na ufuatiliaji wa huduma hizo.
.

Huu ni mpango wa mkakati wa tatu wa shirika hili unaotekelezwa kuanzia mwaka 2022 mpaka 2026 na ni muendelezo wa mipango miwili ya awali huku ukihakikisha mafanikio yaliyotokana na mipango iliyotangulia yanaendelea kuwepo. Mpango huu mpya pia unagu sia mbinu madhubuti zilizobuniwa na kuboreshwa na LSF hapo awali na wakati huo huo ukipitia upya na kuimarisha mbinu mpya zitakazoendana na mabadiliko ya kimazingira na mahitaji ya huduma za msaada wa kisheria. Mabadiliko bayana yanayozingatiwa na mapango huu yanaonekana kwenye sera za serikali na sheria; kusinyaa kwa uhuru; maendeleo ya kiteknolojia na aina mbalimbali za kutoa msaada wa kisheria, pamoja na mabadiliko katika masuala yahusuyo usalama wa binadamu na uhai kwa ujumla hasa matokeo ya Uviko-19; ugaidi; biashara haramu ya usafirishaji binadamu; kukua kwa miji, pamoja na kuhama kwa watu na ukimbizi.

Tofauti kubwa baina ya mpango huu na ile ya awali ni kwamba sasa LSF inalenga zaidi kutekeleza shughuli zake kwa kufuata mfumo unaotoa kipaumbele kwa haki zaidi unaoendana na viwango vya kimataifa na hivyo kujenga mazingira endelevu yanayohakikisha haki inapatikana kwa usawa, vinginevyo ufanisi wa juhudi za kupunguza umasikini na kukuza utawala bora zinakwama (kimsingi hii inamaanisha kuitazama Programu ya Upatikanaji wa Haki katika ujumla wake huku ubora wa huduma za msaada wa kisheria ambazo zimekuwa zikitolewa kwa muongo mmoja uliopita ukitiliwa mkazo).

### Lengo la mpango huu


Mpango huu ni muendelezo wa mafanikio yaliyotokana na muundo na mbinu za utekelezaji wa shughuli za shirika hili huku ukizingatia mabadiliko yanayoibuka, na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza. Mpango huu utaisaidia LSF:

- Kutanua wigo wa shughuli zake kwa ubunifu katika kuwezesha upatikanaji wa haki na huduma za kisheria na kutosheleza mahitaji ya huduma hizo kwa kadri yanavyojitokeza.
- Kuweka mkazo katika matokeo ya shughuli za huduma za kisheria badala ya shughuli zenyewe.
- Kutumia fursa zilizopo kwenye changamoto za upatikanaji wa haki na utoaji wa huduma za kisheria badala ya kukwamishwa na vikwazo.
- Kukuza mazingira ya upatikanaji endelevu wa huduma za kisheria kwa kutumia msingi wa mafanikio ya sasa na ya nyuma.
- Kupitia upya mbinu na njia za upatikanaji wa haki kwa kuzingatia changamoto zilizopo bila ulazima wa kutegemea mikakati isiyo na tija.
- Kuwekeza kwenye matokeo makubwa badala ya mafanikio madogo-madogo.

## Nguzo kuu za mpango huu



LSF inajielekeza katika kutekeleza shughuli zake kwa kufuata mfumo unaotoa kipaumbele kwa haki zaidi unaoendana na viwango vya kimataifa na hivyo kujenga mazingira endelevu yanayohakikisha haki inapatikana kwa usawa.



LSF itawekeza nguvu zaidi kwenye usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa mtoto wa kike, ikilenga hasa kushughulikia kutokuwepo kwa usawa na unyanyasaji, haki za wanawake kwenye umiliki wa ardhi na mali, ukatili wa kijinsia, ushiriki kwenye masuala ya kisiasa, uwezeshwaji na ushirikishwaji kiuchumi, pamoja na upatikanaji wa haki za kiafya.



Mpango huu unaboresha muundo wa utekelezaji wa shughuli za LSF kwa kuhama kutoka kwenye mbinu zilizozoeleka za kutoa msaada wa kisheria na kuelekea kwenye muundo unaotoa kipaumbele kwa masuala ya haki zaidi; unatafsiri upya ukubwa wa shughuli za shirika kwa kuzingatia mbinu jumuishi huku ukitilia mkazo ushirikishwaji, ubora wa viwango vya maisha, ubora katika usimamizi wa fedha (kufanya mambo makubwa kwa fedha kidogo) pamoja na taasisi kuweza kujiendesha.



Kwenye mpango huu LSF imeazimia kuwa mstari wa mbele katika kufanikisha kuwepo kwa jukwaa la ushawishi kwenye ngazi ya taifa na kanda miongoni mwa makundi na mitandao ya wanawake, kwa ajili ya sauti yao ya pamoja na harakati zao ambazo ni muhimu katika kukuza haki za wanawake na watoto wa kike, ikiwa ni pamoja na kujenga mazingira ya upatikanaji wa haki hizi kupitia mifumo rasmi na isiyo rasmi.

## Dira na Dhamira

Miongoni mwa michango muhimu itokanayo na mpango huu mpya ni hatua ya kupitia upya dira na dhima za LSF ili ziweze kuakisi vyema zaidi kazi zetu na mwelekeo wetu katika miaka mitano ijayo.

# Dira

***Jamii ambayo watu wote wana nafasi sawa ya kupata haki.***

# Dhamira

***Kukuza na kulinda haki za binadamu kwa kuboresha uwezeshwaji wa wanawake, watoto wa kike na makundi maalumu kisheria, kijamii, kiuchumi na kiraia kupitia utoaji ruzuku, ushawishi kwenye sera na huduma za msaada wa kisheria.***

## Misingi inayotuongoza

Safari hii zaidi ya kutaja misingi inayotuongoza tu tumeielezea ili kumuwezesha msomaji kupata uelewa wa kina kuhusu LSF inasimamia nini.

### Misingi Inayotuongoza

### Haki

LSF inaamini katika usawa kwenye utekelezaji wa sheria au mamlaka yanayoibeba.

### Usawa

LSF inaamini kuwa binadamu wote ni sawa na wanapaswa kutendewa kwa haki na usawa.

### Uadilifu

LSF inazingatia viwango vya juu kabisa vya maadili katika utendaji wetu wote.

### Uwazi na uwajibikaji

LSF inaamini katika kujiendesha kwa mfumo ulio wazi na inawajibika kwa matendo na maamuzi yake.

### Kujitolea

LSF inawiwa kwenda mbele zaidi katika kuhakikisha inazingatia haki na kuzingatia kuwa watu wote wanapata haki zao bila kuhesabu gharama.

## Malengo makuu ya kimkakati:

### *Lengo la kimkakati la (1):*

**Kukuza upatikanaji wa huduma bora za msaada wa kisheria kwa makundi maalumu hususani wanawake**

Eneo hili la matokeo linalenga kukuzwa kwa upatikanaji wa huduma bora za msaada wa kisheria kwa wanawake na makundi maalumu nchini kote. Kupitia utoaji na usimamizi wa ruzuku huku mkazo ukiwekwa kwa wasaidizi wa kisheria kutumia ubunifu na matumizi ya teknolojia wanawake na makundi maalumu wataweza kupata ushauri wa kisheria, msaada na uwakilishi kwa ubora kulingana na matakwa ya viwango vya huduma hizi.

### *Lengo la kimkakati la (2):*

**Kukuza jamii zenye uelewa wa kisheria hususani wanawake, watoto wa kike na makundi maalumu**

Eneo hili la matokeo linadhihirisha mbinu ya LSF ya uwezeshwaji kisheria kupitia utoaji ruzuku. Linajumuisha matumizi ya maarifa ya jamii katika sheria yatokanayo na uelewa wa sheria na uwezeshwaji unaofanywa na watoa huduma za kisheria na wasaidizi wa kisheria ili jamii iweze kushiriki kutunga na kuboresha sheria na utekelezaji wake, pamoja na kushawishi upatikanaji wa haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi na kijamii, na haki nyinginezo kupitia juhudi za mtu mmoja-mmoja na jamii nzima.

### *Lengo la kimkakati la (3):*

**Kuboresha mazingira wezeshi kwa ajili ya upatikanaji endelevu wa haki**

Eneo hili linaelekeza katika mikakati ya ushawishi inayolenga kurekebisha mapungufu yaliyopo kwenye mfumo wa upatikanaji wa haki; na ushawishi kwa ajili ya kupata sheria, miongozo na marekebisho ya kiutendaji ili mifumo ya sheria iendane na viwango vya kikanda na kimataifa vya upatikanaji wa haki.

### *Lengo la kimkakati la (4):*

**Ukuaji na uendelevu wa LSF na sekta ya msaada wa kisheria**


Lengo hili kwa upande mmoja linazingatia uboreshwaji wa utendaji na uendelevu wa LSF kama taasisi na kwa upande mwingine kuboresha uratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki na watoaji huduma za kisheria kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha huduma hizi zinabaki kuwa endelevu, zenye tija, ufanisi, uwajibikaji na viwango vinavyokubalika.

## Mfumo wa kutathmini matokeo ya shughuli zetu



Kwa miaka mitano ijayo (2022-2026) LSF itatilia mkazo upatikanaji, tathmini na uwasilishaji wa matokeo ya kati kwenye mabadiliko inayotaka kuyaona miongoni mwa **wanawake**, **watoto wa kike** na **makundi maalumu**. Zaidi sana, mpango huu utazingatia ufikiwaji wa mabadiliko hayo ndani ya shirika na sekta ya msaada wa kisheria kama matokeo ya moja kwa moja ya shughuli ilizozifanikisha.

## Nadharia ya mabadiliko




Lengo kuu la LSF ni kukuza upatikanaji wa haki kwa wote hususani wanawake, watoto wa kike na makundi maalumu. Kwenye mpango huu upatikanaji wa haki unatafsiriwa kuwa uwezo wa wanawake, watoto wa kike na makundi maalumu kufikia haki na stahiki zao za kiraia, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Haya yatawezekana kupitia utoaji na usimamizi wa ruzuku ambayo ndiyo hasa kazi ya LSF. Zaidi ya hapo, LSF itafanya juhudi kuboresha ushirikiano, ushawishi, fursa za kujifunza pamoja, na kukuza uwezo wa wadau wake ikijumuisha pia na utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya ruzuku..

**Wastani wa jumla ya USD 34.5 Milioni zitahitajika kati ya mwaka 2022 na 2026 ili kutekeleza mpango huu.**